AZIMIO LA ILO JUU YA KANUNI ZA MSINGI NA HAKI KAZINI NA UFUATILIAJI WAKE

Limepitishwa na
Mkutano wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani
katika kikao chake cha Themanini na Sita,
Geneva, Juni 18, 1998.

UWASILISHAJI

Tarehe 18 Juni, 1998 Shirika la Kazi Duniani (ILO) lilipitisha *Azimio la ILO juu ya Kanuni za Msingi na Haki Kazini na Ufuatiliaji wake* huko Geneva, hivyo kutilia maanani changamoto zinazoletwa na kuingia kwa mfumo wa uchumi huria wa ulimwengu ambazo zimekuwa ndio mwelekeo wa majadiliano mengi katika ILO tangu 1994. Ingawa kuingia kwa mfumo huu wa ulimwengu ni kipengele kinachohusu ukuaji wa uchumi, na ukuaji wa uchumi ni sharti mojawapo la maendeleo ya kijamii, ukweli unabaki kuwa ukuaji huo peke yake hauwezi kuhakikisha maendeleo hayo. Ni lazima ufuatane na kanuni kadha za msingi za kijamii zilizokitwa katika maadili ya pamoja kuwawezesha wote wanaohusika kudai mgao wao wa haki wa mali waliyoizalisha kwa pamoja.

Kusudi la Azimio hili ni kuunganisha nia ya kuhamasisha juhudi za kitaifa ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya kijamii yanakwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi na haja ya kuheshimu tofauti za mazingira, uwezekano na matakwa ya nchi binafsi.

Hatua ya kwanza ya kufikia azma hii ilichukuliwa huko Copenhagen mnamo 1995, ambapo wakuu wa Nchi na Serikali waliohudhuria Kikao cha Viongozi wa Dunia juu ya Maendeleo ya Jamii walikubali masharti maalumu pamoja na Mpango wa Utekelezaji unaohusu "haki za msingi za wafanyakazi" – upigaji marufuku wa kazi za shuruti na ajira kwa watoto, uhuru wa kuunda na kujiunga na vyama, haki ya kuandaa na kujadili maslahi kwa pamoja, mapato sawa kwa kazi sawa na ukomeshaji wa ubaguzi katika ajira. Mkutano wa Mawaziri wa WTO uliofanyika Singapore mnamo 1996 ulitoa fursa ya kuchukuliwa kwa hatua ya pili. Nchi zilihakikisha upya dhamira zao za kuzingatia viwango vya msingi vya kazi vinavyotambuliwa kimataifa, walikumbusha kuwa ILO ni chombo pekee kilichoundwa kushughulikia viwango hivyo na walithibitisha upya kuunga mkono kwao shughuli za kuviendeleza.

Kukubaliwa kwa Azimio kumefanya hatua ya tatu. Kunatoa mchango mkubwa katika madhumuni yaliyowekwa katika aya 54(b) ya Mpango wa utekelezaji uliokubaliwa na Mkutano Mkuu wa Copenhagen, ambao ni kulinda na kuendeleza na kuheshimu haki za

msingi za wafanyakazi, kuomba Nchi zilizoridhia Mikataba ya ILO inayohusika kuitekeleza kikamilifu na Nchi nyingine kutilia maanani kanuni zilizomo humo.

Mifumo ya usimamizi iliyopo inatoa njia za kuhakikisha utekelezaji wa Mikataba katika Nchi zilizoridhia. Kwa zile nchi ambazo hazijafanya hivyo, Azimio linatoa mchango mpya muhimu. Kwanza, linatambua kuwa Nchi Wanachama wa ILO, hata kama hawajaridhia Mikataba inayohusika, wana wajibu wa kuheshimu, "kwa nia njema na kulingana na Katiba, kanuni zinazohusu haki za msingi ambazo ndizo zinazohusika na Mikataba hiyo". Pili, na hiki ndio kipengele cha kwanza cha ufuatiliaji unaotolewa kwenye Kiambatisho cha Azimio, kinajaribu kufikia lengo hili kwa kutekeleza utaratibu wa pekee wa Katiba ya ILO ambapo Nchi zisizothibisha Mikataba ya msingi zinatakiwa kutoa taarifa kila mwaka juu ya maendeleo yaliyofikiwa katika kutekeleza kanuni zilizomo kwenye Mikataba hiyo.

Mwisho, kwa kudhamiria kwa dhati kutumia uwezo wake wa kukusanya raslimali zake za bajeti kufikia malengo ya Mkutano Mkuu wa Copenhagen, Shirika la Kazi Duniani limekwenda hatua moja zaidi. Dhamira hii itaonyeshwa katika taarifa ya dunia ambacho ni kipengele cha pili cha ufuatiliaji kilichopo kwenye Kiambatisho Taarifa ya dunia itatoa kwa jumla maendeleo yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne kwa nchi zilizoridhia Mikataba ya msingi na hata zile ambazo bado hazijaridhia, itatumiwa kama msingi wa kutathmini mafanikio ya utekelezaji katika kipindi kilichotangulia na kama mwanzo wa mipango ya utekelezaji kwa ajili ya misaada ya baadaye.

Kwa kulikubali Azimio hili, ILO imekubali changamoto iliyotolewa na jumuiya ya kimataifa. Imeunda kiwango cha chini cha hali ya jamii katika kukabiliana na ukweli wa kuingia katika mfumo wa uchumi huria wa ulimwengu na inaweza kuangalia mbele kuelekea karne mpya kwa matumaini mapya.

Michel Hansenne

AZIMIO LA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (ILO)
JUU YA
KANUNI ZA MSINGI NA HAKI KAZINI

Kwa kuzingatia kwamba ILO iliundwa kwa kuamini kuwa haki ya jamii ni muhimu kwa ajili ya amani ya kudumu kwa wote;

Kwa kuzingatia kuwa ILO haina budi, hasa sasa, kuangalia kwa jumla uwekaji wake wa viwango, ushirikiano wa kiufundi na uwezo wa kiutafiti katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka yake, hasa ajira, mafunzo ya ufundi na mazingira kazini, ili kuhakikisha kuwa sera za kiuchumi na kijamii zinasaidia kuleta maendeleo mapana na endelevu, katika muktadha wa mkakati wa kiulimwengu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

Kwa kuzingatia kuwa ILO haina budi kutilia maanani zaidi matatizo ya watu wenye mahitaji maalumu ya kijamii, hasa wasiokuwa na kazi na wafanyakazi wahamaji, na kuhamasisha juhudi za kimataifa, kikanda na kitaifa zinazolenga katika kutatua matatizo yao, na kuendeleza sera zinazofaa zenye nia ya kuongeza ajira;

Kwa kuzingatia haja ya kuweka uhusiano baina ya maendeleo ya kijamii na ukuaji wa kiuchumi, kuhakikisha kanuni za msingi na haki kazini ni jambo lenye umuhimu maalum kwa kuwa kunawezesha wahusika kudai kwa uhuru na kwa misingi ya fursa sawa haki ya mgao wao wa mali waliyosaidia kuizalisha, na kufikia uwezo wao kamili wa kibinadamu katika kufanya mambo;

Kwa kuzingatia kwamba ILO ni shirika la kimataifa lenye haki ya kikatiba na ndio chombo chenye uwezo wa kuweka na kushughulikia viwango vya kazi vya kimataifa, na linaungwa mkono kiulimwengu na linatambuliwa katika kuendeleza haki za msingi kazini kama njia ya kudhihirisha kanuni zake za kikatiba;

Kwa kuzingatia ni muhimu, katika hali ya kutegemeana kwa uchumi unaokua, kuthibitisha upya kutobadilika kwa kanuni za msingi na haki zilizopo katika Katiba ya Shirika na kuendeleza matumizi yake ulimwenguni kote;

Mkutano wa kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani,

1. Unakumbusha:

(a) Kwa kujiunga kwa hiari na ILO, Wanachama wote wamekubali na kuidhinisha kanuni na haki zilizowekwa na katiba yake na Azimio la Philadelphia, na wamekubali kujishughulisha katika kufikia malengo ya jumla ya Shirika kulingana na uwezo wa raslimali walizo nazo na mazingira waliyomo;
(b) kwamba kanuni na haki hizi zimeelezwa na kuendelezwa katika muundo wa haki na wajibu maalumu katika Mikataba inayoatambuliwa kuwa ni msingi ndani na nje ya Shirika.

2. Unatangaza kuwa Wanachama wote, hata kama hawajaridhia Mikataba inayohusika, wana wajibu, kutokana na uanachama wao, kuheshimu, kukuza na kutambua, kwa nia njema na kulingana na Katiba, kanuni zinazohusu haki za msingi ambazo ndio chanzo cha Mikataba hiyo, yaani:
   (a) uhuru wa kujiunga na kuunda vyama na kutambua kikamilifu haki ya mapatano ya pamoja;
   (b) ukomeshaji wa aina zote za kazi za shuruti na za kulazimishwa;
   (c) ukomeshaji kamili wa ajira ya watoto; na
   (d) ukomeshaji wa ubaguzi katika ajira na kazi.

3. Unatambua wajibu wa Shirika katika kusaidia Wanachama wake, kulingana na mahitaji yao yaliyopo na yaliyoelezwa, ili kufikia malengo kwa kutumia katiba yake kikamilifu, raslimali za uendeshaji na bajeti, ikiwa pamoja na raslimali na misaada kutoka nje, pamoja na kuhamasisha mashirika mengine ya kimataifa ambayo ILO ina uhusiano nayo, kulingana na Ibara 12 ya Katiba yake, kuunga mkono juhudi hizo:
   (a) kwa kutoa ushirikiano wa kiufundi na huduma za ushauri kuendeleza uridhishaji na utekelezaji wa Mikataba ya msingi;
   (b) kwa kusaidia Wanachama ambao hawajaridhia baadhi au Mikataba yote katika juhudi zao za kuheshimu, kukuza na kutambua kanuni zinazohusu haki za msingi ambazo zimo katika Mikataba hiyo; na
   (c) kwa kusaidia Wanachama katika juhudi za kuweka mazingira yanayoruhusu maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

4. Unaamua kwamba, ili kulipa nguvu za utekelezaji Azimio hili, ufutiliaji wa kuliendeleza, ambao ni wa maana na unaofaa, utatekelezwa kulingana na hatua maalumu zilizo kwenye kiambatisho kilichomo humu, ambacho kitachukuliwa kama sehemu ambatani ya Azimio hili.

5. Unasisitiza kuwa viwango vya kazi havitatumiwa kama kigezo cha kushiriki katika biashara ya kimataifa, na kwamba hakuna sehemu yoyote ya Azimio hili itakayotumika kwa nia hiyo; na pia, manufaa ya ziada ya nchi moja hayatahusishwa na Azimio hili na ufuatiliaji wake.

Kiambatisho

Ufuatiliaji wa Azimio

I. Nia ya Jumla

1. Nia ya ufuatiliaji unaoelezwa hapa chini ni kuhamasisha juhudi zinazofanywa na Wanachama wa Shirika kuendeleza kanuni na haki za msingi zilizopo katika Katiba ya ILO na Azimio la Philadelphia na kusisitizwa tena katika Azimio hili.

2. Kulingana na lengo hili, ambalo ni la makusudio ya kimaendeleo, ufuatiliaji huu utawezesha kutambuliwa kwa maeneo ambayo msaada wa Shirika unahitajika kupitia shughuli za ushirikiano wa kiufundi ambao utaonekana unafaa katika kuwasaidia Wanachama kutekeleza kanuni na haki za msingi. Hata hivyo, hauwi badili ya mifumo ya usimamizi iliyopo, na wala hautazuia utekelezaji wake; hivyo hali maalumu zilizopo katika mifumo hiyo hazitachambuliwa kulingana na ufuatiliaji huu.

3. Vipengele viwili vya ufuatiliaji huu, vilivyoelezwa hapo chini, vinatokana na utaratibu uliopo: ufuatiliaji wa kila mwaka unaohusu Mikataba ya msingi ambayo haijaridhiwa utakuwa na maana ya kukubali njia za sasa za kutekeleza ibara 19, aya 5(e), ya Katiba; na taarifa ya dunia itatumika kupata matokeo bora ya utaratibu uliotekelezwa kwa mujibu wa Katiba.

II UFUATILIAJI WA KILA MWAKA WA MIKATABA YA MSINGI ISIYORIDHIWA

A. Nia na mawanda

1. Nia ni kutoa fursa ya kutathmini kila mwaka, kwa kutumia utaratibu rahisi badala ya tathmini ya miaka minne iliyoanzishwa na Bodi yaUtawala mnamo 1995; juhudi zinazofanywa na Wanachama ambao hawajaridhia Mikataba yote ya msingi kulingana na Azimio hili.

2. Ufuatiliaji utakuwa kila mwaka katika maeneo manne ya kanuni na haki za msingi zilizoelezwa katika Azimio.

B. Njia

1. Ufuatiliaji utatokana na taarifa zilizoombwa kutoka kwa Wanachana kulingana na Ibara 19 aya (5) (e) ya Katiba. Fomu za taarifa zitatayarishwa ili kupata habari kutoka serikali ambazo hazijaridhia Mkataba au Mikataba ya msingi, kuhusu mabadiliko yoyote katika sheria au utekelezaji wao, kwa kutilia maanani ibara 23 ya Katiba na taratibu za utekelezaji zilizopo.

2. Taarifa hizi, kama zitakavyokusanywa na Ofisi, zitaangaliwa upya na Bodi ya Utawala.

3. Ili kutoa utangulizi kwa ajili ya taarifa zilizokusanywa, kutanabahisha juu ya kipengele chochote kinachohitaji majadiliano ya kina, Ofisi inaweza kutumia kikundi cha wataalamu kilichoteuliwa kwa ajili hiyo na Bodi ya Utawala.

4. Marekebisho ya taratibu zilizopo za Bodi ya Utawala ni lazima yachunguzwe ili kuwawezeshaWanachama wasiowakilishwa kwenye Bodi ya Utawala kutoa maelezo yanayohitajika au yanayofaa wakati wa majadiliano ya Bodi ya Utawala ili kutoa habari zaidi kutokana na taarifa zao, kwa njia inayofaa.

III. TAARIFA YA DUNIA

A. Nia na Mawanda

1. Nia ya taarifa hii ni kutoa picha dhahiri ya dunia inayohusu kila kipengele cha kanuni na haki za msingi kilichoonekana katika kipindi cha miaka minne iliyotangulia, na kutumika kama msingi wa kutathmini manufaa ya msaada unaotolewa na Shirika, na kwa ajili ya kuweka vipaumbele kwa kipindi kinachofuata, kwa kutumia muundo wa mipango ya utekelezaji kwa ajili ya ushirikiano wa kiufundi ulioundwa maalumu kwa ajili ya kukusanya raslimali za ndani na nje zinazohitajika kuuendeleza.
2. Kila mwaka, taarifa itahusu kipengele kimojawapo cha vile vinne vya kanuni na haki za msingi, kwa zamu.

B. Njia

1. Taarifa itatolewa chini ya uangalizi wa Mkurugenzi Mkuu kwa misingi ya taarifa rasmi, au habari zilizokusanywa na kutathminiwa kulingana na taratibu zilizowekwa. Kwa zile Nchi ambazo hazijaridhia Mikataba ya msingi, habari zitatokana hasa na matokeo ya ufuatiliaji wa kila mwaka ulioelezwa awali. Kwa Wanachama ambao wamekwisharidhia Mikataba inayohusika, taarifa itatokana hasa na taarifa kama zinavyoshughulikiwa kulingana na ibara 22 ya Katiba.

2. Taarifa hii itawasilishwa kwenye Mkutano mkuu wa Shirika la Kazi Duniani kwa ajili ya majadiliano ya pande tatu kama taarifa ya Mkurugenzi Mkuu. Mkutano unaweza kushughulikia taarifa hii peke yake bila taarifa nyingine zinazotokana na ibara 12 ya Kanuni Kuu, na wanaweza kuijadili katika kikao kinachohusu taarifa hii tu, au kwa njia yoyote ile inayoonekana inafaa. Hapo itakuwa ni kazi ya Bodi ya Utawala, katika kikao chake cha karibu, kuhitimisha mjadala kutokana na majadiliano haya juu ya vipaumbele na mipango ya utekelezaji kwa ajili ya ushirikiano wa kiufundi utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka minne inayofuata.

IV. INAELEWEKA KWAMBA

1. Mapendekezo yatatolewa kwa ajili ya marekebisho ya Kanuni Kuu za Bodi ya Utawala na Mkutano mkuu ambazo zinahitajika kutekeleza masharti yaliyoelezwa hapo awali.

2. Mkutano mkuu utaangalia upya, kwa muda unaofaa, utekelezaji wa ufuatiliaji huu kutokana na uzoefu uliopatikana ili kutathmini kama umetimiza vya kutosha dhamira ya jumla iliyoelezwa katika Sehemu I.

Kilichotangulia ni Azimio la ILO juu ya Kanuni na Haki za Msingi Kazini na Ufuatiliaji wake lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani katika Kikao chake cha Themanini na Sita ambacho kilifanyika Geneva na kufungwa rasmi Juni 18, 1998.

KWA NIA NJEMA tunaambatisha saini zetu siku hii ya kumi na tisa ya Juni 1998

Rais wa Mkutano
JEAN-JACQUES OECHSLIN

Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi
MICHEL HASNSENNE